# HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE

**.................................**

Nukushi: 028 -2227148
Simu: 028 -2227140
E- Mail: karagweded@yahoo.com

S. L. P. 20,
KARAGWE.

01/06/2017

Kwa Vyombo vya Habari,
Wilaya ya
**KARAGWE.**

**YAH: MADA FUPI KUELEKEA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI TAREHE 5, JUNE 2017.**

Rejea kwenye mada tajwa hapo juu,

Tafadhari Wilaya pokeeni mada fupi inayohusu maadhimisho ya siku ya mazingira Duniani yatakayofanyika tarehe 05/06/2017. Kwakuwa maadhimisho ufanyika kwa kuhamasisha wananchi naomba nitumie fursa hii kufikisha ujumbe wa siku hii kwa wananchi wa Karagwe na Mkoa kwa ujumla

Asanteni.

## 1.0 UTANGULIZI

Kila tarehe 5 Juni, kila mwaka Watanzania tunaungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliamuliwa na Baraza la Umoja wa Mataifa la mwaka 1972,wakati wa Mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa uliohusu Mazingira huko Stockholm, nchini Sweden. Aidha, Azimio la kuunda Shirika la Umoja wa Mataifa la kushughulikia Mazingira Duniani, yaani United Nations Environment Programme (UNEP) lilipitishwa pia siku hiyo. Tangu wakati huo, nchi mbalimbali duniani zimekuwa zikiadhimisha Siku ya Mazingira Duniani kila mwaka tarehe 5 Juni, kwa ujumbe maalumu unaotolewa na Umoja wa Mataifa.

## 1.1 Dhumuni la Siku ya Mazingira Duniani.

Madhumuni ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ni kuhamasisha jamii duniani kote kuelewa masuala yahusuyo Mazingira na pia kuhamasisha watu wa jamii mbalimbali duniani kuwa mstari wa mbele katika kuchukua hatua za kuhifadhi na kulinda mazingira.

Aidha, tunatumia siku hii kutoa fursa kwa jamii kufahamu kwamba wao wana wajibu wa kuzuia madhara na mabadiliko hasi katika Mazingira na kuhamasisha jamii kufanya mazingira yao kuwa salama na masafi ili sote tufurahie hali hiyo katika maisha yetu na vizazi vyetu.

Kwa Mwaka 2017, kimataifa maadhimisho haya tanafanyika nchini Canada. Maamuzi ya kupeleka maadhimisho haya nchini Canada ni kutokana na nchi hiyo kuwa na maeneo mengi yenye mazingira asili ya ardhi na maji ukilinganisha na nchi zingine. Kitaifa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yatafanyika katika kijiji cha Butiama, Mkoani Mara, kwa ajili ya kumuenzi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (Baba wa Taifa). Kwa upande wa mkoa wa Kagera, maadhimisho haya yatafanyika Wilaya ya Muleba wakati Kiwilaya yatafanyika kata ya Rugera kwenye viwanja vya shule ya msingi Omukakajinja.

## 1.2 Kaulimbiu ya Maadhimisho mwaka huu

Kaulimbiu inayoongoza maadhimisho haya kimataifa ni "Connecting People to Nature". Kwa Kiswahili ni: "Mahusiano Endelevu Kati ya Binadamu na Mazingira". Kaulimbiu hii inahamasisha wananchi kuwa na urafiki endelevu na mazingira asilia ambapo kila mtu anapaswa kutambua, kufurahi, kujivunia na kulinda uzuri wa mazingira asilia yetu na kuhamasishana kuyatunza na kuhifadhi.

Pamoja na kaulimbiu ya kimataifa, kaulimbiu yetu ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira mwaka huu kitaifa ni "**Hifadhi ya Mazingira: Muhimili kwa Tanzania ya Viwanda."** Serikali yetu imeamuatuwe na kaulimbiu hiyo ili kuhamasisha utunzaji wa mazingira wakati tunapokuza maendeleo ya viwanda hapa chini kwetu. Wananchi wa Tanzania

tunahimizwa kutunza mazingira yetu hasa tunapoingia kwenye kipindi hiki cha mageuzi ya viwanda kwani viwanda tunavyotarajia kuanzisha vinategemea maliasili na mazao mbalimbali katika kuzalisha na kujiendesha. Zaidi ya hili, Viwanda vingi vimebainika kuwa mstari wa mbele katika kuchafua na kuharibu mazingira yetu ya ardhi, maji na hewa.

Mara kwa mara tumeshuhudia katika uzalishaji wa viwanda mazingira asilia huharibiwa sana, hususan, kwa taka zitokanazo na uzalishaji na utupwaji wake. Hivyo basi, kaulimbiu ya kitaifa inahimiza wazalishaji viwandani kuzingatia usimamizi endelevu wa taka zitokazo viwandani, uzalishaji wa bidhaa kwa viwango vinavyotakiwa na utumiaji endelevu wa bidhaa zinazozalishwa viwandani. Utiririshwaji ovyo wa maji machafu na utupaji ovyo wa taka za viwandani umepelekea kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa mazingira asilia, hususan, ardhi maji na hewa. Kaulimbiu hii kitaifa inahamasisha wamiliki wa viwanda na wazalishaji wa bidhaa za viwandani washiriki kikamilifu katika kutunza na kuhifadhi mazingira asili kwa kuhifadhi na kutupa taka kwenye maeneo husika na kuondoa sumu kwenye maji machafu yatokanayo na uzalishaji viwandani.

Kimsingi kwa tafsiri ya haraka kauli mbiu hii inamaanisha kuwa tunapofikiria kuazisha viwanda tufikirie kabisa kuendelea kuhifadhi mazingira yetu kwa kasi zaidi huku tukiendeleza zoezi la Tathmini ya Athari za Kimazingira kwa lengo la kudhibiti athari hasi zinazoweza kujitokeza wakati wa uazishaji,undeshaji na uzalishaji wa viwanda. Hivyo yatupasa kutumia vyema rasilimali zetu zilizopo kuendeleza viwanda vyetu kwa njia endelevu kwa ajili ya manufaa ya kizazi cha sasa lakini pia kwa kizazi cha kesho.

## 2.0 SHUGHULI ZINAZOHARIBU MAZINGIRA

Dunia kwa sasa inakabiliwa na changamoto za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Chanzo kikubwa cha tatizo hili ni shughuli za kibinadamu. Katika nchi zilizoendelea, uchafuzi huu unatokana na shughuli za viwandani, hususani uzalishaji na matumizi ya nishati itokanayo na makaa ya mawe na mafuta, wakati nchi

zinazoendelea, tatizo hili linachangiwa na; uharibifu wa misitu; uzalishaji na utupaji taka hovyo; kilimo na ufugaji usiozingatia kanuni za uhifadhi; makazi holela; uchimbaji wa madini; ukosefu ama kutokufuata mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na shughuli za viwandani.

Mojawapo ya matokeo ya shughuli hizi ni kuongezeka kwa gesi joto ambalo limepelekea pamoja na mambo mengine, mabadiliko ya misimu ya mvua; ukame; mafuriko; ongezeko la wadudu waharibufu (wa mazao na magonjwa ya binadamu ama mifugo); kuongezeka ama kupungua kwa kina cha maji ya bahari, maziwa, mito na mabwawa; uharibifu wa vyanzo vya maji; upotevu wa makazi ya viumbehai n.k.

Sote tunafahamu kwamba zipo nchi hapa duniani zilizoharakisha maendeleo ya viwanda bila kuzingatia kanuni za uhifadhi wa mazingira na leo tunaona jinsi ambavyo wanahangaika kusafisha kwa gharama kubwa hewa na majiyaliyochafuliwa. Tunashuhudia katika nchi hizo kwamba kuna nyakati shule zinafungwa, Maduka na Ofisi zinafungwa na wananchi wanarazimishwa kutotoka nje ya nyumba zao ama kufunika pua na midomo yao kwa sababu hewa imechafuka kupita kiasi kutokana na moshi wa viwandani. Kwa kuwa tumeona gharama hiyo kubwa ya uchafuzi wa mazingira, ni muhimu sisi tukajifunza na kutofanya makosa waliyoyafanya wenzetu.

Kwa msingi huo, serikari yetu imetoa wito kwa wamiliki, wazalishaji wa viwanda, pamoja na wananchi wote kwa ujumla kutumia fursa ya maadhimisho haya kuhakikisha maendeleo ya viwanda hayaathiri mazingira asilia ya nchi yetu ambayo ni hazina ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Kwa sasa kuna changamoto inayolikumba taifa letu ambayo ni mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na ukweli kuwa, nchi zilizoendelea kama Ulaya na Marekani ndizo zimechangia kwa kiasi kikubwa katika tatizo hili, lakini ukweli ni kwamba, nchi zinazoendelea ndio waathirika wakubwa wa madhara ya mabadiliko ya tabianchi ikiwemo Tanzania. Hii inatokana na uwezo mdogo wa kiuchumi wa nchi hizi kukabiliana na madhara haya.

Maeneo mengi ya nchi yetu tayari yamekumbwa na tatizo hili. Kwa mfano, hivi leo kiwango cha maji katika maziwa, Mito, vijito na mabwawa katika maeneo mengi nchini kinazidi kupungua. Mfano mzuri ni hapa Wilayani Karagwe ambapo sisi wenyewe tumeshuhudia vyanzo vyetu vya maji vikikauka , tumekuwa na kiangazi cha muda mrefu na kusababisha ukame mkubwa ulioleteleza njaa kubwa kiasi cha kuletewa msaada wa chakula hapa Karagwe kwa mara ya kwanza . Tumeshuhudia sisi wenyewe mifugo mbalimbali ikifa kwa kukosa malisho na maji huku tukikubwa na magonjwa mbalimbali ya binadamu (malaria), Mifugo (MFD) pamoja na magonjwa ya mimea kama myauko wa migomba na kahawa (unyanjano).

Maeneo mengine ya nchi yetu yameendelea kuwa makame huku maeneo mengine yakinyemelewa na jangwa. Maeneo mengine yamekumbwa na ongezeko la wadudu waharibufu wa mazao na/ama magonjwa ya binadamu na mifugo. Vilevile, maeneo mengi ya nchi yetu yamekumbwa na tatizo la kubadilika kwa misimu ya mvua na hivyo kuathiri mzunguko wa uzalishaji mazao.

## 3.0 NINI KIFANYIKE KUTIMIZA DHANA YA MATUMIZI ENDELEVU

Haya ni matatizo yanayoonekana au kuhisiwa kutokana na shughuli za binadamu wanapotumia/wasipotumia vizuri rasilimali zilizopo katika mazingira yao ama mahali ambapo shughuli zao zinafanyika mfano kwenye Kaya, Kitongoki, Kijiji Kata au Wilaya. Hivyo, jitihana na mbinu mahususi za kukabiliana na matatizo ya ki mazingira zinaitajika mfano :

- **Kufanya Tathimini ya Athari za Mazingira**
    - **Tathimini ya Athari za Mazingira(TAM)** ni mbinu za kubaini matatizo ya kimazingira yanayoweza kujitokeza kutokana na miradi ya kijamii au kimaendeleo. Shughuli hii hutakiwa kufanywa kabla ya mradi au kabla ya shughuli kuanza katika kiwango chochote.
- Kuzingatia masuala ya matumizi bora ya ardhi za vijiji

  - Hii usaidia kutenga matumizi mbalimbali ya raslimali kama malisho, kilimo, misitu, vyanzo vya maji, makazi na madini yaliyopo.
- Kuzingatia sera, sheria na miongozo ya kilimo, ardhi, mifugo, mazingira,ujenzi na makazi, uzazi wa mpango.
- Kuzingatia masuala ya usafi wa mazingira kwa kusimamia utupaji taka ovyo, utirishaji wa maji taka na usafi wa vyoo na makazi.
- Kuzingatia mbinu mbadala za kukabiliana na mataokeo ya mabadiriko ya tabia nchi kwa kufanya shughuli ambazo ni za kujikinga kama:
  - Kuchimba visima virefu katika maeneo kame ili kurahisisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu, kilimo, na mifugo;
  - Kuboresha mifumo ya tahadhari ili kuepusha madhara yatokanayo na majanga yanayohusishwa na mabadiliko ya tabianchi;
  - Kusaidia upatikanaji wa nishati jadidifu kwa wananchi.
  - Kurudisha uoto wa asili uliopotea kwa kupanda miti mingine, kutumia nishati mbadala kama pumba, matmizi ya majiko banifu na kuhifadhi misitu ya asili kwa njia shirikishi (CBFM).
- Kujiunga kwa wanajamii kwenye mpango wa MKUHUMI (REDD+) wa kuzilipa fidia nchi ambazo zinapanda miti na kutunza misitu inayosaidia kupunguza hewa ya ukaa na kuhamasika zaidi kutunza misitu ilyopo na kupanda miti mingine zaidi.

## 3.1 Kwanini Tunaadhimisha Kiwilaya Kata Ya Rugera

Tumechakua kufanya maadhimisho haya kata ya Rugera kwani kata hii imepakana na mamlaka ya Mji mdogo Kayanga ambapo tunaetegemea kupata wawekezaji mbalimbali wa kuanzisha viwanda hapa Wilayani. Lakini pia kata ya Rugera inao bado uoto wa asili amabopo ukihifadhiwa vizuri kutakuwepo na msitu wa asili ambao utatumika kama chijio (carbon sink) ya hewa ya ukaa itakayokuwa inazalishwa mjini.

Zaidi ya hayo , serikari za vijiji vya kata hii zina mpago wa kuhifadhi misitu yao ya kijiji kwa njia ya pamoja (Joint Forestry Management). Hii itasaidia

kuzuia uharibifu wa misitu ya kwa kukata miti kwa ajiri ya mikaa, kuni na mbao lakini pia kusaidia kudhibiti matukio ya uchomaji moto hovyo.

Hivyo siku ya maadhimisho huko Rugera zitafanyika shughuli zifuatazo; usafi wa mazingira kwenye Kaya, zahanati, shule na eneo la gulio kwa kufyeka nyasi na vichaka na kuchoma takataka, pia kutakuwepo upandaji wa miti ya kumbukumbu , usafi wa chanzo cha maji pamoja na kuelimisha wanachi juu ya shughuli za uhifadhi wa misitu ya asili, udhibiti wa uchomaji moto ovyo, Ufugaji holela wa mifugo na ukataji miti ovyo kwa ajili ya shughuli za uchomaji Mkaa na tofali.

**MWISHO:**

**Busara duniani inatwambia :-** Mazingira yapo kwa ajili ya viumbe wote duniani sisi binadamu hatukupewa Dunia hii sisi peke yetu bali na viumbe wengine. Binadamu hatumiliki sayari ya dunia, ila tunaishi humo. Katika hili tunapaswa kutumia rasilimali zilizopo kwa njia endelevu kwakuwa katika dunia si kwamba rasilimali hizi hazina mwisho, la asha zinaisha.Hivyo baadhi ya mikakati ya maendeleo inakubalika, mingine haikubaliki, maendeleo endelevu yanapendelewa zaidi hivyo basi wasio wa baba wa Taifa wa 1961 unaosema kuwa maeneo yanayohifadhiwa yaendelee kuhifadhiwa na yeyote atakayevunja sheria tupambane naye kwa sababu anatufanyia jambo la dhambi utuongoze .

Ahsante sana

Mada hii imeandaliwa na

**P. R. RWEYENDERA**
**AFISA USAFI NA MAZINGIRA (W)**
**<u>KARAGWE</u>**